# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 106 (h) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012 na majukumu yake yametajwa katika kifungu cha 114 kama ifuatavyo:

a) Kufuatili utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viogozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati, ahadi za Serikali,kazi za kawaida na za maendeleo ,ukusanyaji wa mapato na matumizi pamoja na kufanya ziara katika Taasisis za Serikali za Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora
- Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Aidha, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nane katika mizunguko minne kama ifuatavyo:-

i) Unguja wiki mbili tarehe 13 hadi tarehe 24 Mei 2013
ii) Dar-es- Salaam wiki mbili kuanzia tarehe 09 hadi tarehe 20 Septemba 2013.
iii) Pemba wiki moja kuanzia tarehe 18 hadi 22 Novemba 2013 na Unguja wiki moja kuanzia tarehe 25 hadi tarehe 29 Novemba 2013.
iv) Unguja wiki mbili kuanzia tarehe 30 Disemba 2013 hadi tarehe 10 Januari 2014.

Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Kamati imeundwa na Wajumbe wafuatao:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma - Makamo M/ kiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg. Makame Salim Ali - Katibu

Kamati ilifanya kazi zake kwa kutumia Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Hansard za Baraza, Hotuba za bajeti za Taasisi za Wizara za Serikali za mwaka 2013/2014 pamoja na taarifa za taasisi husika za Serikali.

## SEHEMU YA PILI

## OFISI YA RAIS IKULU NA UTAWALA BORA

Oofisi hii imeundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
3. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
4. Idara ya Mawasiliano - Ikulu
5. Idara ya uendeshaji na Utumishi
6. Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO)
7. Ofisi ya Ofisa Mdhamini - Pemba
8. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje
9. Idara ya Utawala Bora
10. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi
11. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
12. Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini
13. Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi

14. Idara ya Ukuzaji Uchumi
15. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

**OFISI YA OFISA MDHAMINI - PEMBA**

**CHANGAMOTO:**

Katika Ofisi hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Tatizo la usafiri. Bado ofisi hii inakabiliwa na uhaba wa gari za kutosha hasa pale inapotokea viongozi wetu wanapokwenda Pemba.

2. Ufinyu wa bajeti. Bado ni tatizo na kwa namna moja ama nyengine linachangia kutofikiwa kwa baadhi ya malengo waliyojipangia.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati imeridhishwa na hatua zilizofikiwa katika ukarabati wa Ikulu ya Mkoani lakini pia kamati inataka Ofisi ya Rais kushuhulikia kwa haraka suala la ujenzi wa uzio kwa lengo la kuimarisha usalama wa Ikulu hiyo.

2. Pia kamati inaiagiza Ofisi ya Rais kushuhulikia suala la kuzuia athari ya mmongo'nyoko wa ardhi uliopo katika Ikulu ya Mkoani.

3. Kamati inaridhishwa na inapongeza hatua iliyofikiwa kwa upande wa Unguja kwamba Ikulu zote pamoja na majengo yake yameshapatiwa hatimiliki. Hata hivyo kwa upande wa Pemba bado suala hili halijashughulikiwa ipasavyo, hivyo Kamati inaiagiza Ofisi hii kuwasiliana na Wizara ya Ardhi kuharakisha utoaji wa hatimiliki za majengo hayo.

4. Aidha Kamati imeridhishwa na maendeleo ya matengenezo ya jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Wete Pemba na kuona hatua iliyofikiwa. Hivyo Kamati inatoa wito ya kuongezwa kwa bajeti ya Ofisi hii ili iweze kukamilisha hatua za ujenzi zilizosalia.

5. Kamati pia inaendelea kusisitiza kwa mara nyengine tena kuharakishwa kwa ujenzi wa Ofisi ya Rais huko Pemba kutokana na ukosefu wa Ofisi uliopo kwa muda mrefu ambao umekuwa ukisumbua utendaji kazi wa Ofisi hiyo.

6. Kamati inatoa agizo kwa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kumaliza ujenzi wa Rest House ya Micheweni iliyosita kujengwa kwa kipindi kirefu.

**IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE (DIASPORA)**

Licha ya uhaba wa fedha unaotokana na bajeti finyu wanayopatiwa Idara hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha.

**CHANGAMOTO:**

Changamoto kubwa inayoikabili Idara hii ni ukosefu wa fedha unaopelekea Idara kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi unaotakikana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Ili kufanikisha utekelezaji mzuri wa majukumu yao ambao utakuwa na tija kwa jamii na nchi yetu Kamati inapendekeza yafuatayo:-

1. Idara hii inahitaji kutengewa bajeti ambayo itaiwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi.

2. Kuna umuhimu mkubwa kwa jamii kuelimishwa kuhusu suala la "Diaspora" ambalo lina umuhimu wake katika masuala ya uchumi.

**IDARA YA UTAWALA BORA:**

Kamati ilipatiwa taarifa za utekelezaji wa majukumu yaliyo chini ya Idara ya Uutawala Bora kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

**CHANGAMOTO ZA IDARA YA UTAWALA BORA:**

Kamati ilikutana na Idara hii ya Utawala Bora na kubaini changamoto kadhaa wanazokabiliana nazo licha ya jukumu kubwa na zito la kusimamia masuala yote ya Utawala Bora katika nchi yetu ambazo ni:-

1) Ufinyu wa Bajeti
2) Uhaba wa nafasi katika jengo la Ofisi wanayofanyia kazi kwa sasa.
3) Ukosefu wa usafiri ambapo kwa sasa wana gari moja tu ya Mkurugenzi nayo haiko katika hali nzuri.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kamati inashauri yafuatayo ili kufanikisha majukumu ya Idara hii:-

1. Kutenga fedha maalum kwenye bajeti ijayo kwa ajili ya ununuzi wa gari itakayosaidia ufuatiliaji wa kazi.

2. Kuongeza fedha za bajeti kwa lengo la kuielimisha jamii masuala ya Utawala bora. Hili lina umuhimu wake kwa kuzingatia kuwa nchi yetu

inakabiliwa na matukio mawili (2) makubwa yanayohitaji kupatiwa elimu hii ili yawezwe kutekelezwa kwa ufanisi. Matukio hayo ni kura ya maoni kuhusu upatikanaji wa katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano na Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar na Tanzania wa Mwaka 2015.

3. Kuna haja na ulazima wa kushughulikia kesi za udhalilishaji wa watoto ili ile dhana ya Utawala Bora iweze kufanikiwa, na hii zaidi ni katika utolewaji wa haki katika sehemu za Mahakama kwa kesi hizi.

4. Kamati inaitaka Idara hii kuwajibika ipasavyo ili uhuru wa kusema katika masuala ya dini na siasa usitumiwe vibaya na kuwadhuru wengine.

**MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangiwa kwa mujibu wa sheria.

**CHANGAMOTO:**

Licha ya majukumu mazito waliyopewa taasisi hii na nchi bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo kwa namna moja ama nyengine huenda zikakwamisha utekelezaji uliokusudiwa wa majukumu yao:-

1. Ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi
2. Uhaba wa maslahi ikiwemo mshahara pamoja na posho nyeti(mazingira maalum ya kazi zao)
3. Ukosefu wa usafiri katika kufutilia mambo mbalimbali.
4. Upungufu wa wataalamu hasa katika fani za uchunguzi na sheria.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kamati inapendekeza yafuatayo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa:-

1. Kuangalia uwezekano wa kuipatia Ofisi za kisasa mamlaka hii zinazoendana na kazi zake, kwani kwa mujibu wa kazi zao wanatakiwa wawe na chumba maalum na madhubuti (*strong room*) kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka na mambo mengine ya kiuchunguzi.

2. Kuboresha maslahi ya wafanyakazi kiujumla pamoja na posho la mazingira maalum kupitia *sheme of service* yao.

3. Kuwapatia usafiri wa uhakika pamoja na vitendea kazi vya kutosha wafanyakazi ili wamudu vyema majukumu yao.

4. Kuwapatia watendaji mafunzo maalum ya kiuchunguzi ndani na nje ya nchi ili kufanya kazi zao kwa ufanisi.

5. Kuandaa programu maalum na kuziwasilisha kwa wafadhili kwa lengo la kuisaidia mamlaka masuala mbali mbali yakiwemo mafunzo kwa watendaji pamoja na vitendea kazi.

6. Kushirikiana na taasisi za nchi nyenginezo zinazohusika na udhibiti wa rushwa kwa lengo la kubadilishana mawazo na kujenga uzoefu.

7. Kamati inawaomba watumishi wa Mamlaka kuwa wazalendo zaidi na kuweka mbele maslahi ya nchi kwanza lakini pia kufanya kazi zao kwa uadilifu wa hali ya juu bila ya kukubali kushawishiwa na mtu yeyote.

8. Kamati inaishauri Mamlaka ya Kuzuia Rushwa kujenga ushirikiano mkubwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika utekelezaji wa kazi zao kwa lengo la kuongeza nguvu na ufanisi wa kudhibiti rushwa.

9. Ofisi ya Rais kusimamia na kutekeleza kwa haraka suala la ulinzi katika eneo la Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa kwa kuvitumia Vikosi vya SMZ.

**OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeendelea kuwajibika katika kusimamia nidhamu ya matumizi ya rasilimali za serikali pamoja na mashirika yake kisheria.

**CHANGAMOTO:**

Pamoja na mafanikio ambayo tumeanza kuyaona lakini Kamati imebaini changamoto zifuatazo kwa Ofisi hii:-

1. Uhaba wa usafiri ikiwemo gari na vipando vyengine katika kufuatialia kazi mbalimbali.

2. Upungufu wa wafanyakazi. Mfano Ofisi ina Mwanasheria mmoja tu lakini pia kwa upande wa *Zonal Auditor* mmoja anahudumia Wizara sita (6) kitu ambacho kwa namna moja ama nyengine kinarudisha nyuma kasi ya utendaji kazi.

3. Upungufu wa wataalamu. Licha ya juhudi zinazochukuliwa na Ofisi hii lakini bado wataalamu wanahitajika katika nyanja tofauti ili kumudu vyema majukumu yake.

4. Uhaba wa maslahi. Ingawa watendaji wa Taasisi hii hufanya kazi kubwa ya kudhibiti fedha za umma na kuhakiki kuwa fedha hizo zinatumika vizuri maslahi yao ni madogo na kupelekea baadhi ya watumishi kukimbilia katika Taasisi nyenginezo. Hali hii inazorotesha kazi za ukaguzi na udhibiti wa fedha za umma.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea Ofisi ya CAG bajeti kwa lengo la kuipatia usafiri.

2. Kamati inaishauri serikali kuharakisha muundo wa Utumishi wa Ofisi ya CAG ili iwe ni motisha kwao kufanya majukumu yao ya Kikatiba kwa ufanisi mkubwa.

3. Kamati pia inazishauri taasisi nyengine za Serikali kupitia Ofisi ya CAG kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo mambo ya *security* ya ofisi, udhibiti wa vifaa na rasilimali za ofisi, *promotion* na *motivation* pamoja na *retention* ya rasilimali watu.

4. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Ofisi ya CAG kisheria ili iwe na uwezo wa kuchukua hatua zaidi za kiushahidi mbele ya kesi inazozithibitisha kuhusu matumizi mabaya ya fedha za umma.

5. Kamati pia inaishauri Serikali kuishirikisha kikamilifu Ofisi ya CAG katika mradi wa *e-government* katika ngazi ya kitaalamu ili waweze kujua kinachofanyika na kuweza kufanya kazi kwa urahisi pindi watakapohitaji taarifa zinazowahusu katika mkongo huo.

6. Kamati aidha inaishauri Ofisi ya CAG kuanza kufanya *Technical Auditing* hasa kwenye miradi ya barabara, madaraja na majengo mengine ili kujiridhisha kutokana na ubora wake. Pia Kamati inashauri Ofisi hii ianze kufanya tathmini ya kitaalamu kuweza kujua hasara inayopata Serikali kutokana na tabia ya kucheleweshwa kukamilishwa kwa miradi mbalimbali nchini ikiwemo ya barabara na mengineyo.

7. Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais kuiangalia upya sheria iliyompa mamlaka Mdhibi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili taarifa zake ziweze kuwa ni sehemu ya ushahidi.

8. Kamati imeitaka Ofisi ya Mdhibiti kuishauri ZRB kuacha kukusanya mapato kwa njia ya fedha taslim na badala yake kutumia njia ya benki ambayo iko salama zaidi.

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1) Kamati inashauri kuwepo na mashirikiano mazuri na ya karibu baina ya taasisi zinazohusika kupitia Idara ya Uratibu wa mambo ya Muungano ili kutatua changamoto ziliopo.

**2)** Kamati inaishuri Ofisi hii kuielimisha jamii masuala yanayohusu takwimu zinazohusiana na mfumko wa bei ili jamii iwe na ufahamu kuhusu kupanda na kushuka kwa bei za bidhaa.

**MAAGIZO YA KAMATI KWA (OR) IKULU NA UTAWALA BORA/ SERIKALI**

1. Kamati inatoa agizo la kumalizwa kwa utata juu ya suala la Ikulu ya Micheweni kwani ni muda mrefu sasa kumekuwa na kauli ya mazungumza na muhusika. Kamati imeona ni vyema kuchukuliwa hatua za haraka kulimaliza suala hili.

2. Kamati inatoa agizo kwa Wizara husika kushirikiana na wahusika wote ikiwemo watu wa ardhi kuharakisha utoaji wa hatimiliki za majengo haya kwa upande wa Pemba.
3. Pia kamati inaiagiza Ofisi ya Rais kushughulikia suala la kuzuia mmongo'nyoko wa ardhi uliopo katika Ikulu ya Mkoani hasa upande wa nyuma ya jengo.
4. Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais Ikulu kulisimamia suala la Ikulu ya Mkokotoni na kujengwa fensi.
5. Kamati inaitaka Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kuandaa mradi ambao utaweza kushughulikia ukarabati pamoja na mmog'onyoko wa ardhi unaosababishwa na maji chumvi uliopo katika eneo la Ikulu ya Bwefumu.
6. Kamati inaagiza kukamilishwa kwa scheme of service ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia Ofisi ya Rais.
7. Kamati pia inataka kuangaliwa upya sheria iliyompa mamlaka CAG ili taarifa zake ziweze kuwa ni sehemu ya ushahidi.
8. Kamati imeiagiza Ofis Ikulu na Utawala Bora ya Rais kusimamia na kutekeleza suala la ulinzi katika eneo la ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.
9. Kamati inaiomba Serikali kumpatia haki zake Mkurugenzi wa Mamlaka hii kama sheria inavyoelekeza. Aidha, Kamati inaomba Serikali kumpatia usafiri Mkurugenzi huyu ili aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.
10. Kamati imeitaka Ofisi ya Mdhibiti kuwashauri ZRB kuachana na tabia ya kukusanya mapato ya serikali kwa njia ya mkononi.

**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaundwa na Ofisi na Idara zifuatazo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
3. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
4. Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali
5. Idara ya Maafa
6. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa
7. Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali
8. Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar-es-salaam
9. Baraza la Wawakilishi
10. Tume ya Uchaguzi
11. Ofisi Kuu Pemba.

**OFISI YA FARAGHA**

Ofisi ya Faragha imeendelea na majukumu yake ya msingi ya kutoa huduma zinazostahiki kwa Mhe Makamu wa Pili wa Rais.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuchukua hatua za kufunga CCTV kamera katika Ofisi ya Mhe Makamo wa Pili wa Rais kwa lengo la kuimarisha usalama.

2. Kamati yangu inaiomba serikali kuu kuliangalia suala la ujenzi wa nyumba za Viongozi wetu wakuu wa Kitaifa hasa kule Pemba, kwani Kamati haikuridhika na jinsi wanavyoshughulikiwa wakiwepo kisiwa cha Pemba, hasa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais. Aidha, hawana usafiri wa kutosha kwa kisiwa cha Pemba jambo ambalo hulazimika misafara yao kusitisha shughuli nyingi za kikazi wakati wanapokuwepo Pemba kwani magari mengi ya mawizara huazimwa kwa ajili ya kuwahudumia viongozi hao pamoja na misafara yao.

3. Vile vile kamati inaishauri Serikali kujenga jengo jengine Dodoma ambalo litaendana na hadhi ya Mhe Makamu wa Pili wa Rais, lakini pia na Dar-es Salaam kujengwa jengo la nyumba ya Mhe Makamu wa Kwanza na wa Pili ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

4. Kamati yangu pia inashauri kwa upande wa Zanzibar kuhamisha ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kujengwa jengo jengine la kisasa litakalokuwa na huduma zote na eneo lenye faragha. Sio pale lilipo hivi sasa.

**IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI**

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Kamati inaridhishwa kwa kiasi juu ya Uratibu wa Shughuli za serikali unavyofanywa hivi sasa lakini inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuimarisha uratibu huo na kufikia dhamira na malengo pamoja na mategemeo ya wananchi kwa nchi yao.

1. Serikali ihakikishe utekelezaji wa taarifa za Kamati za Kudumu, na Kamati Teule za Baraza zinafanyiwa kazi ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kuwa na imani na Serikali yao kwani maelezo yanayotolewa Barazani mengi huwa yanatoka kwa wananchi na utekelezwaji wa maagizo hayo ndio kuwatumikia wao.

   Vile vile kuna ubadhirifu mwingi uliogundulika na Kamati zilizoundwa na Baraza la Wawakilishi lakini hatuoni hatua za haraka kuchukuliwa, hii itapelekea wale wakosaji kujihisi wako sawa na wengine kuweza kufanya kama hivyo kwani watahisi kufanya ubadhirifu ni jambo la kawaida tu. Hivyo hata malengo ya Serikali itakuwa ni ndoto tu ikiwa tutaendelea kuoneana muhali huku wachache wakiitafuna nchi,

Kamati inaamini ikiwa Serikali itakuwa makini basi bado kuna uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa bajeti ya matumizi ya kawaida kupitia mapato yetu ya ndani bila kutegemea wafadhili kutoka nje.

2. Kamati imeona kwa kuwa kuna malalamiko na migogoro mingi ya ardhi, Kuna umuhimu mkubwa kwa waratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuifuatilia kwa karibu na kumshauri ipasavyo Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi kwani miongoni mwa kadhia kubwa iliyopo hapa Zanzibar ni unyang'anywaji wa Ardhi, unyanyaswaji wananchi na wawekezaji hasa walioekeza katika maeneo ya pwani, suala hilo hasa katika kuwazuia wananchi kuzitumia fukwe na kuwafungia njia za kuelekea pwani kwenye shughuli zao za kila siku za kutafuta rizki.

3. Kamati inamuomba Mhe. Makamu wa pili wa Rais akiwa yeye ndiye kiongozi wa shughuli za siku zote za serikali awe mkali na kuchukua maamuzi magumu na sahihi ili kulikomesha suala hili la malalamiko ya ardhi kwani wale wavamizi wamekuwa na kibri kwa kuona serikali haiwezi kuchukua hatua dhidi yao jambo ambalo wananchi hawaridhiki nalo. Kamati imeshuhudia barua nyingi za malalamiko ya wananchi zinazopelekwa serikalini lakini zinazopatiwa ufumbuzi ni chache sana.

4. Ili kutekeleza vyema suala zima la Utawala Bora na kuzifanya Taasisi tatu za Nchi kwa maana ya Mahkama, Chombo cha Kutunga Sheria na Serikali kutekeleza kazi zao bila ya kuingiliana, ni vyema Mahkama ya Ardhi ikawekwa chini ya Mahkama Kuu badala ya utaratibu wa sasa, Mahkama hiyo kuwa chini ya wizara inayoshughulikia utoji na uhaulishaji wa ardhi. Hii ni kutokana na malalamiko yaliyopo ya ucheleweshaji wa kesi unaosababishwa na watendaji wa wizara.

**IDARA YA MAAFA**

Kamati inaipongeza Idara hii ya Maafa kwa kujitahidi kutekeleza majukumu kwa kadri ya hali inavyoruhusu.

**CHANGAMOTO ZA IDARA YA MAAFA:**

Mbali na kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:-

1. Upungufu wa vifaa vya kutendea kazi. Kimsingi inaonekana Idara hii kazi yao kubwa ni ya kuwaunganisha tu ( *coordination*) wadau mbalimbali wa maafa ikiwemo KVZ, KMKM na wadau wengine, lakini kwa upande wa kuwajenga uwezo kivifaa bado ni changamoto kubwa kwao.

2. Ucheleweshaji wa kupata taarifa wakati ajali ama maafa yanapotokea. Hali hii wakati mwengine huchangia katika kufanya maafa yawe makubwa kuliko kama taarifa ingepatikana mapema.

3. Kukosekana kwa sheria inayokwenda na wakati itakayosaidia kutekeleza shughuli za uratibu wa mambo ya maafa kwa ufanisi zaidi. Hivi sasa sheria iliopo ya mwaka 2003 inaonekana haitoi nafasi nzuri zaidi katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

4. Uhaba wa fedha unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa Mfuko wa Maafa, hii ni kusema kwamba kwa sasa Idara hii inategemea utaratibu wa kawaida wa fedha za O/C katika kuendesha shughuli zake. Ijapokuwa sheria ya mwaka 2003 imetaja suala la kuanzishwa mfuko wa maafa lakini cha kusikitisha mpaka sheria hii inataka kufanyiwa marekebisho bado mfuko huo haujaanzishwa.

5. Ukosefu wa vifaa kwa Idara ya maafa Pemba, hii ni kutokana na kwamba vifaa vyote vya Idara hiyo huwepo Makao Makuu Unguja. Kwa namna moja ama nyengine hali hii inazorotesha hali ya uokozi pale maafa yanapotokea Pemba.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri serikali kuipatia Idara hii vifaa vya kutosha na vya kisasa ili iweze kukabiliana na maafa pindi yanapotokea. Kamati pia katika hili inaishauri Serikali kusadiana na kushirikiana na wawekezaji binafsi mfano wa muwekezaji kwenye sekta ya ufundishaji wa kurusha ndege kwani ana vifaa na ndege ambazo zinaweza kutua hata juu ya bahari. Hili kwa mazingira ya nchi linaweza kutusaidia na faida ikapatikana kwa pande zote mbili.

2. Kamati pia inashauri kuwa taarifa za ajali au maafa zitolewe kwa haraka kwa lengo la kuwahisha uokozi na kupunguza maafa.

3. Kamati inashauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuharakisha kuwasilisha Barazani Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maafa ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sheria hiyo na kuondoa kwa lengo la kuondoa vikwazo vinavyokwamisha utekelzaji mzuri wa kazi za Idara.

4. Kmati vile vile inaishauri Serikali kuitekeleza sheria hiyo kwa kuanzisha kwa vitendo Mfuko wa Maafa ulioanishwa katika sheria hiyo. Kuwepo kwa mfuko huo kutaiwezesha idara kuondokana na utaratibu wa sasa wa kutegemea fedha za O/C ambazo kiukweli hazitoshelezi kwa asilimia kubwa katika utekelezaji wa Mfuko huo.

5. Kamati pia inaishauri Serikali kuijengea Idara ya Maafa jengo la kisasa na kuipatia vitendea kazi ili kuharakisha utoaji wa huduma pale maafa yanapotokea.

6. Mbali na hayo Kamati pia inashauri suala la elimu ya Maafa lipewe kipaumbele kuanzia ngazi ya awali, shehia na hadi maofisini ili wananchi waelewe jinsi ya kukabiliana na maafa pale yanapotokea.

7. Kamati pia inakumbushia kusaidiwa katika masomo na matunzo kwa watoto ambao waliondokewa na wazee wao katika ajali ya *Spice Islander* lishughulikiwe ipasavyo.

**IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA**

Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Mhe Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa kuadhimisha na kufannikisha sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi.

Aidha Kamati inatoa shukrani za dhati kwa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa chini ya Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Maandalizi na Uratibu wa Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi nzuri waliyoifanya.

**CHANGAMOTO:**

Hata hivyo Idara hii nayo inakabiliwa na changamoto kuu zifuatazo:-

1. Uhaba wa vitendea kazi. Hii inajumuisha vifaa vyote vya upambaji ikiwemo mashamiana na vifaa vyengine vinavyofana na hivyo.
2. Uhaba wa vyombo vya Usafiri.
3. Ufinyu wa bajeti. Zaidi hili ndilo linalozaa changamoto zilizotangulia hapo juu.
4. Maslahi duni kwa watendaji.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa vitendea kazi vya kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
2. Kamati pia inaiomba Serikali pale zinapotokea kazi na sherehe za Kitaifa kuhakikisha kuwa stahiki za watendaji wa Idara hii zinalipwa kwa wakati.
3. Kamati pia inaishauri Serikali katika suala la uhifadhi wa kumbukumbu za Viongozia Wakuu wa Kitaifa kuhakikisha kunakuwa na Nyumba Maalum ya makumbusho kwa ajili hiyo ili uhifadhi uwe mzuri na endelevu kwa faida ya vizazi vijavyo na historia ya nchi.

**IDARA YA UPIGAJI CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI:**

Kamati ilitembelea Idara ya Kiwanda cha Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Maruhubi na kuridhishwa kwa kiasi kikubwa na hatua zilizofikiwa katika kuimarisha Idara, lakini pia ilibaini changamoto zifuatazo:-

a) Licha ya kufungwa kwa mashine mpya na za kisasa za Uchapaji bado kuna upungufu wa vitendea kazi jambo ambalo linategemewa kukamilishwa katika awamu ya pili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

b) Changamoto nyengine ni utaratibu wa Kuhama kutoka Saateni kuelekea Maruhubi umesababisha nyaraka kuachwa Saateni.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais kukifanya kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Shirika ili kiweze kujiendesha wenyewe.

2. Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa kuzihifadhi na kuzitunza vizuri nyaraka za Serikali kwa faida ya nchi. Kmati pia inatilia mkazo kuwa nyaraka zilizoachwa katika kiwanda cha zamani Saateni zihamishiwe Maruhubi kwa faida ya Sserikali na jamii kwa ujumla. Sote tunaelewa umuhimu wa nyaraka si kwa sasa tu bali hata kwa siku za usoni. Utaratibu wa sasa kuziacha nyaraka Saateni na kuhamia Maruhubi si sahihi hata kidogo bali lazima nyaraka hizo zichukuliwe vizuri ama kama zitabakia Saateni basi pia zihifadhiwe vizuri na ulinzi pia wa nyaraka hizo uwepo tena wa kutosha.

**IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ - DAR-ES-SALAAM:**

Kamati katika kipindi cha mwezi wa Septemba ilipata nafasi ya kuzitembelea taasisi zifuatazo Tanzania Bara kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali lakini pia ikiwa ni sehemu ya kutekeleza majukumu yake. Taasisi zilizotembelewa ni pamoja na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Chuo cha Polisi Moshi, TPDC, Songosongo Kilwa, JKT Makao Makuu na SUMA JKT.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

Katika ziara ya Kamati sehemu zote hizo Kamati inapenda kushauri yafuatayo kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zake:-

a. Kamati inashauri kuwa suala la itikadi za kidini linalopelekea uvunjifu wa amani lisimamiwe ipasavyo na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa yeyote atakayesababisha machafuko.
b. Kamati inashauri suala la tindikali( acid) lifanyiwe jitihada za makusudi kwa kudhibitiwa ipasavyo ili lisije likasababisha athari za mipasuko ya kidini.
c. Kamati pia inasisitiza kuangaliwa upya na kwa uzito unaostahiki suala la eskoti za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa upande wa Zanzibar kwa vile ziko katika hali mbaya ili kuepusha athari na maafa yasiyotegemewa kwa viongozi wetu pamoja na nchi kwa ujumla.
d. Kamati inashauri katika kiwanja cha ndege cha Kisauni, kuwe na watendaji wataalamu wa kudhibiti dawa za kulevya kwa lengo la kupunguza janga hilo.
e. Kwa upande wa bodaboda Kamati inashauri kutungwa sheria ambayo itaweza kudhibiti utumiaji wa vyombo hivyo pamoja na umiliki wake kwa ajili ya kupunguza ajali na uhalifu ambao unafanywa na watumiaji wa bodaboda.

f. Aidha Kamati inashauri kushughulikiwa suala la meli ya Tanzania iliyokamatwa na madawa ya kulevya huko Italia kwa vile inaharibu jina la Tanzania.

g. Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wataalamu wake kuwa tayari kwenda kujifunza katika nchi zenye uzoefu juu ya mambo mbalimbali yanayohusu utafutaji wa mafuta na gesi.

h. Kamati imeshauri kuendelea kwa ushirikiano uliopo kati ya JKU na JKT ili kusaidia maendeleo na kupiga hatua kwa JKU Zanzibar.

i. Kamati pia imeomba kusaidiwa vijana wa JKU Zanzibar katika suala zima la elimu ya uzalishaji mali ili nao waweze kufikia lengo la kupunguza umasikini na kuongeza kipato.

j. Kamati inashauri deni la mkopo wa matrekta 50 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo ambapo waliingia mkataba wa kukopa lilipwe ili kuondosha usumbufu usio wa lazima.

k. Aidha Kamati inavishauri vikosi vya ulinzi vya SMZ kuanzisha kampuni za ulinzi ambazo zitakuwa zinatoa huduma za ulinzi binafsi kwa mashirika, kampuni na hata mahoteli ambapo Zanzibar utalii ndio pato la nchi.

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Ofisi ya Baraza kuwa na maandilizi ya kutosha kuhusu Bunge la Katiba kwa kuwapatia Wajumbe rasimu ya pili pamoja na elimu juu ya rasimu hiyo.

2. Kamati pia inashauri taratibu zote za lazima zifanywe ili Mheshimiwa Spika aweze kuhamia katika nyumba iliyojengwa maalum kwa ajili yake. Kamati inaona kuendelea kukaa tu kwa nyumba ile bila ya kutumiwa ni kupoteza gharama kubwa zilizokwishatumika.

3. Kuhusu Ofisi za Baraza Pemba Kamati inaomba kufanyiwa ukarabati zaidi pamoja na kuwepo huduma zote ili iweze kutumika. Aidha Kamati inatoa pongezi kwa matengenezo makubwa yaliyofanywa hadi sasa, lakini pia kuna kazi kubwa ya kufanywa mpaka Ukumbi wa Baraza uweze kufanya kazi zake zilizokusudiwa.

4. Kamati inaishauri na kuisisitiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Serikali kulishughulikia suala la echo katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi pamoja na jengo zima la Baraza.

**TUME YA UCHAGUZI:**
Tume ya Uchaguzi Zanzibar imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangiwa ikiwemo kuboresha daftari la kudumu la kupiga kura kwa kuorodhesha wapiga kura wapya na kutoa wale wasiofaa kuwemo kwa mujibu wa sheria kupitia mikoa yote Unguja na Pemba.

**CHANGAMOTO:**

Mbali na utekelzaji wa majukumu yake kamati ilibaini changamoto ifuatazo katika Tume ya Uchaguzi:-

Kamati ilibaini Tume ya Uchaguzi haikuingiziwa fedha mwaka 2011, 2012 Wajumbe wa Tume walikuwa wanamaliza muda wao, hivyo kusababisha zoezi la Uandikishaji kuchelewa hadi Juni 2013 baada ya Tume mpya kuundwa tarehe 30 Aprili 2013.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Tume ya Uchaguzi Zanzibar kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuepusha vitendo vya uvunjifu wa amani hasa katika vipindi vya Uandikishaji na Uchaguzi wenyewe.

2. Aidha Kamati inapenda kuishauri Tume kaunza kutoa elimu ya uraia kwa wananchi na kujua haki zao na mipaka yao kwa mujibu wa sheria. Elimu hii zaidi juu ya masuala yanayohusu mambo ya Uchaguzi.

**OFISI KUU PEMBA**
Kamati ilitembelea Pemba katika kipindi cha Novemba 2013 na kubaini changamoto zifuatazo:-

a) Uingizwaji wa fedha za O/C usioridhisha kwa upande wa Pemba (Julai-Septemba 2013, (27%)

b) Ukosefu wa nyumba/makaazi pamoja na upungufu wa gari/usafiri kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

c) Ucheleweshaji usio na sababu za msingi wa Uajiri kwa upande wa Pemba unaosababishwa na Tume ya Utumishi Serikalini kushindwa kutoa vibali vya ajira hizo zisizopungua 11 kwa karibu miaka 2 sasa.

d) Ukosefu wa vifaa kwa Idara ya maafa Pemba, hii ni kutokana na kwamba vifaa vyote vya Idara hiyo huwepo Makao Makuu Unguja.

e) Bado kuna tatizo la ucheleweshaji usio na sababu za msingi wa utolewaji hatimiliki za majengo mbali mbali hata pale malipo yake yanapokamilika.

f) Kukosekana kwa Ofisi za Mhe Spika na Katibu katika jengo la Baraza Pemba, Aidha, kuna ukosefu wa chumba cha wageni.

g) Kasoro za wazi katika nyongeza ya mishahara ya watumishi. Kiwango cha jumla cha 25000 bila ya kuzingatia kiwango cha elimu na uzoefu wa kazi kina kasoro na hakiwapi ari watumishi bali kinadumaza ari zao ikiwa ni pamoja na kujenga matabaka na chuki zisizo za ulazima katika maofisi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inashauri Jengo la Baraza la Wawakilishi Pemba lifanyiwe marekebisho makubwa ili vikao vya Baraza viweze kufanyika Pemba, kinyume na hivyo kwa hali ilivyo sasa vikao haviwezi kufanyika Pemba.

2. Kamati pia inashauri suala la maji katika nyumba ya Mhe Spika litafutiwe ufumbuzi wa haraka kwani bila ya maji nyumba haikaliki.

3. Aidha Kamati inaendelea kushauri juu ya suala la usafiri na makaazi kwa Viongozi Wakuu lazima liekewe bajeti yake maalum na litekelezwe kwa umakini na uangalifu mkubwa kwani makaazi ni stara na si busara kuendelea utaratibu unaotumikahivi sasa.

4. Kamati inaikumbusha Tume ya Utumishi Serikalini kukamilisha zoezi la uajiri wa nafasi zote zilizoombwa na Ofisi ya Makamu wa Pili Pemba. Ili kuharakisha maendeleo ya Ofisi hii.

5. Elimu ya maafa itolewe kwa wananchi wote kupitia Shehia zao ili lile lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa. Kwani maafa yanayowakumba ni watu, hivyo ni vyema mkazo ukawekwa katika kuwapa elimu hasa wale walioko vijijini ili waweze kukabiliana na Maafa mbalimbali pale yanapotokea.

6. Elimu juu ya uendeshaji wa miradi hasa ya TASAF III itolewe kwani ni nyenzo muhimu sana ili kufanya miradi hiyo kuwa yenye tija na endelevu na mwishowe kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuondosha umaskini nchini.

**MAAGIZO YA KAMATI KWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS:**

a. Kamati imelitaka Jeshi la Polisi kutoa agizo kwamba vituo vya Polisi isiwe sehemu ya mahakama bali iwe ni njia tu ya kuelekea mahakamani, na hili zaidi katika kesi za udhalilishaji.

b. Kamati pia imeagiza suala la makaazi ya Polisi liwekewe mpango maalum wa kukabiliana na tatizo hilo, lakini pia Kamati imeona wakati umefika sasa wa kujenga Makao Makuu mapya ya Jeshi la Polisi kwa Zanzibar yanayoendana na hadhi na wakati wa sasa.

c. Kamati inataka kuzingatiwa suala la Ujenzi wa kituo cha Polisi katika Uwanja wa Ndege mpya kwani ni muhimu sana kiusalama wa nchi na watu wake

d. Kamati inaishauri Serikali kulichukulia uzito suala la Idara ya Maafa, kwani inaonekana haipewi uzito kama vile inavyotakikana. Na hili ikiwa na pamoja na uanzishwaji wa Mfuko wa Maafa.

e. Kuhusiana na jali ya boti ya Kilimanjaro II, kamati inaiomba Serikali kutoa taarifa maalum, sahihi na kamili juu ya ajali hiyo ili kuondoa dhana ambazo zimejengeka kwa baadhi ya watu ndani ya jamii.

f. Jengo la Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba liiimarishwe ili liweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

g. Kamati inatoa agizo kwamba fedha zote za o/c kwa upande wa Pemba ni lazima zipelekwe Pemba tena kwa wakati na kwa kiwango kile kile kilichoidhinishwa na Baraza ili kazi ziweze kufanyika kama zilivyopangwa.

h. Tume ya Utumishi Serikalini ikamilishe zoezi la uajiri wa nafasi zote zilizoombwa na Ofisi ya Makamu wa Pili Pemba haraka iwezekanavyo.

i. Kamati inaitaka Wizara Kilimo kufuatilia deni inayodaiwa SMZ kupitia Wizara ya Kilimo la matrekta 50 kutoka JKT liweze kulipwa kabla ya mwaka huu wa bajeti kumalizika.

j. Kamati aidha inataka suala la *escort* za viongozi kuangaliwa upya na kwa umakini zaidi ili kuhakikisha usalama wa viongozi wetu.

k. Kamati inaiagiza Ofisi ya Baraza kukamilisha Rasimu ya Mswada wa Utawala wa Baraza Kwa lengo la kuimarisha Baraza la Wawakilishi liweze kujitegemea na kujiendesha katika kazi zake.

**OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zifuatazo:-

a) Ofiisi ya Faragha
b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
c) Idara ya Uendeshaji na Utumishi
d) Idara ya Mazingira
e) Idara ya Watu Wenye Ulemavu
f) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba
g) Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya
h) Tume ya Ukimwi.

Kamati ilifuatilia Utekelezaji wa Bajeti, Miradi, Sera na Ukusanyaji wa Mapato katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Unguja na kubaini changamoto mbali mbali zikiwemo hizi zifuatazo:-

1. Wananchi bado wanavuna mali asili zisizorejesheka bila ya kufuata Sheria na Utaratibu wa Kimazingira.

2. Bidhaa chakavu kama vile magodoro, nguo na vifaa vya umeme visivyokuwa na viwango bado vinaendelea kuingizwa kwa kasi nchini bila ya utaratibu.

3. Hakuna Utaratibu wa Ufuatiliaji wa athari za Kimazingira kabla ya kuanza Utekelezaji wa Miradi mbali mbali hasa mikubwa kwa hapa nchini. Hata ile miradi ambayo taratibu zinafuatwa basi kunakuwa na ukiukwaji wa makusudi wa maagizo na ushauri unaotolewa na Idara ya Mazingira kwa taasisi husika.

4. Uingizwaji na Utumiaji wa dawa za kulevya bado upo na unaendelea kwa kasi nchini na kuendelea kuiathiri jamii.

5. Mabadiliko ya Tabia nchi yanaendelea kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii huku idadi kubwa ya jamii hawafahamu athari zake, ama hawana elimu ya kutosha juu ya athari za mabadiliko hayo kwa maendeleo yao binafsi na nchi kwa ujumla.

6. Udhalilishaji wa watu wenye ulemavu bado unaendelea katika jamii.

7. Kuhusu ujenzi wa *Rehabilitation centre,* Suala hili limekuwa ni la muda mrefu jambo ambalo linawakosesha vijana wanaoacha kutumia madawa ya kulevya kupata pahala pa kurejesha hali na afya zao. Ijapokuwa ucheleweshwaji huo unatokana na ufinyu wa bajeti, lakini Serikali lazima ioneshe nia ya dhati kabisa katika kufanikisha suala hili.

8. Kamati imebaini changamoto zilizopo baina ya mwekezaji wa Sea Cliff Hotel iliyopo Nyanjale na wananchi wa eneo husika. Mwekezaji huyo kupitia mwakilishi wake alikiri kuwepo kwa changamoto hizo na kuahidi mbele ya Kamati kwamba atashirikiana kikamilifu na Mwakilishi wa Jimbo husika katika kutatua changamoto hizo.

## TUME YA UKIMWI

Kamati inaipongeza jitihada zinazofanywa na Tume ya Ukimwi kutokana na kazi kubwa wanayoifanya katika kupambana na kudhibiti maambukizi mapya ya maradhi ya Ukimwi na pia elimu wanayoitoa kwa jamii inasaidia sana kujikinga na maambukizi mapya ya maradhi ya Ukimwi.

Aidha Kamati yangu inazipongeza NGO'S zote zinazotoa elimu ya mapambano dhidi ya maradhi ya Ukimwi kwani bila wao basi hali ingekuwa ni mbaya sana, kwani kazi wanazozifanya hasa kuwasaidia wagonjwa walioko majumbani ni kazi kubwa sana na inastahiki kupongezwa na tunawaomba kuongeza bidii ili kupunguza maambukizi mapya.

**CHANGAMOTO:**

Pamoja na kazi yote ya mapambano haya inayofanywa bado Tume ya Ukimwi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Upungufu wa fedha za wahisani za kuendeleza mapambano ya UKIMWI hali ambayo huenda ikasababisha kupungua kwa juhudi za wananchi na taasisi mbali mbali katika mapambano dhidi ya KIMWI.

2. Kuwepo kwa unyanyapaa ndani ya jamii ambalo hupelekea watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kukosa haki zao.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fungu kubwa zaidi katika bajeti ya kila mwaka kwa kuweza kusaidia mapambano ya maambukizi mapya dhidi ya gonjwa hili hatari la Ukimwi, na hili litafanikiwa tu pale itakapoweza kuendelea kutolewa elimu kwa wananchi kila itapobidi.

2. Kamati pia inaishauri Tume ya UKIMWI kutumia vyema fedha zote zinazotolewa ikiwa na Serikali ama zile za wafadhili kwa madhumuni ya kufikia lengo lililokusudiwa la kuwasaidia watu wanaoishi na virusi vya ukimwi pamoja na kutoa elimu kwa umma na si vyenginevyo.

**IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU**

Kamati inapongeza Idara hii kwa kazi kubwa inayoifanya hasa kuwatambua na kutetea haki zao watu wenye ulemavu, lakini pia kusaidiana na asasi za kiraia katika kuwapatia huduma pamoja na mafunzo mbali mbali ili kujiunga pamoja na kutetea haki zao.

**CHANGAMOTO:**

Idara ya Watu wenye Ulemavu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Udhalilishaji wa watu wenye ulemavu.
2. Tatizo la ajira kwa watu wenye ulemavu.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inashauri kuangaliwa kwa kina suala la ajira kwa watu wenye ulemavu kwani wapo baadhi yao wana uwezo mzuri wa kufanya kazi.

2. Kamati inashauri pia kuchukuliwa hatua suala la udhalilishaji wa watu wenye ulemavu ambalo bado linazidi kuongezeka kila siku ndani ya jamii yetu.

## IDARA YA MAZINGIRA

Idara ya mazingira inaendelea na jitihada za kuhakikisha utunzaji wa mazingira unaendelea ili kuzuia athari zisizo za lazima kutokea. Mbali na jitihada hizo idara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO:**

1. Uharibifu wa mazingira bado ni tatizo ndani ya jamii.
2. Jamii kuendelea kuvuna rasilimali zisizorejesheka bila ya kufuata taratibu za uhifadhi wa mazingira.
3. Athari za mabadiliko ya tabia ya nchi na kuathiri shughuli za wananchi kwenye kilimo, huduma ya maji ya kunywa na uvuvi.
4. Ukosefu wa jengo la Ofisi ya Idara ya Mazingira.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Kamati inasisitiza kuangaliwa suala la upatikanaji wa Ofisi ya Mazingira kwani jengo wanalotumia hivi sasa haliridhishi kutokana na udogo wa jengo lenyewe pamoja na uhaba wa nafasi ambao ni tatizo kubwa katika kutekeleza kazi zao.

2. Kamati pia inashauri kufanyiwa marekebisho ya haraka sheria ya mazingira ili kuweza kupunguza athari zinazoendelea kujitokeza pamoja na kuipa nguvu sheria katika utekelezaji wa kazi za mazingira. Kutokana na umhimu huo Kamati inashauri kuharakishwa mchakato wa kupatikana kwa Sheria ya Mazingira ambayo itakuwa chachu ya kupunguza uharibifu unaotokea hivi sasa, lakini pia sheria ambayo itaweka usimamizi mzuri wa rasilimali mbalimbali za nchi na kuziendeleza kulingana na matakwa ya kimazingira.

3. Kamati pia imebaini udhaifu mkubwa kwa upande wa ZIPA katika kutekeleza na kusimamia sheria ipasavyo, hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hupewa vibali hata kabla ya kufanyiwa tathmini ya kimazingira jambo ambalo ni kinyume na sheria. Hivyo Kamati inatoa wito tabia hii iachwe mara moja kwa maslahi ya nchi na kuwataka waweke mbele maslahi ya nchi kuliko maslahi yao binafsi, kwani janga lolote litakapotokea watakaopata hasara ni Zanzibar na wazanzibari na si wawekezaji.Tunalizungumza hili zaidi kwenye miradi ya mahoteli na miradi mingine mikubwa ya uwekezaji.

4. Kamati pia inaiomba serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji kuwaangalia wananchi wa Uwandani kwani kazi wanayoifanya ya ukataji wa matofali ya mawe ni hatari kwa afya zao, hivyo waangalie namna ya kuwawezesha ili kuendesha shughuli zao kwa uzuri. Na hii ni ahadi ya Mhe Rais pamoja na Mhe Makamu wa Kwanza wa Rais walipotembelea eneo lile kwa nyakati tofauti.

**TUME YA URATIBU NAUDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA**

Tume imeendelea na jukumu la kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Hata hivyo Tume inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO:**

1. Kuendelea kwa uingizwaji na utumiaji wa madawa ya kulevya.
2. Kuongezeka kwa vitendo viovu ndani ya jamii ambavyo hurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

**MAONI YA KAMATI:**

1. Ugumu na ukubwa wa kukabiliana na tatizo unatokana zaidi na ukubwa wa mtandao wenyewe. Hivyo Kamati yangu inashauri kuwe na ushirikiano wa pamoja na kuundwe kikosi maalum kuanzia ngazi ya shehia ili kuwabaini wale wote wanaojihusisha na biashara ama matumizi ya dawa hizi za kulevya.
2. Kamati pia inaitaka jamii kusaidia katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kwa kuwafichua wahusika wanaoendelea kuharibu vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa letu.

**OFISI KUU PEMBA**

Ofisi ya Makamo wa Kwanza Pemba imeendela kutekeleza majuku yake kama ilivyopangiwa lakini bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

**CHANGAMOTO:**

1. Ofisi inakabiliwa na ufinyu wa bajeti jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linachangia kutofanya vizuri sana hasa kwenye kazi za ufuatiliaji na utekelezaji wa mambo mbalimbali ikiwemo suala la mazingira.

2. Ofisi pia inakabiliwa na uhaba wa usafiri. Suala hilo pamoja na ufinyu wa bajeti imepelekea shughuli za uendeshaji pamoja na ufuatiliaji wa uharibifu wa mazingira kuwa na mashaka.

3. Sheria ya Mazingira haitoi fursa kwa Idara ya Mazingira kudai fidia baada ya kuzuia ujenzi unaofanywa na muwekezaji aliyekwenda kinyume na sheria. Hali hii imeipelekea Idara ya Mazingira, Pemba baada ya kuzuia ujenzi wa Hoteli ya Muyuni Makangale, na maeneo mengine kushindwa kudai fidia ya aina yoyote baada ya hoteli hiyo kuanza ujenzi bila ya Kufanyiwa Tathmini ya Mazingira.

4. Uharibifu wa Mazingira bado unaendelea na ni jambo la kusikitisha kuona mpaka leo bado kuna taasisi za Serikali zinazoshiriki moja kwa moja katika uharibifu huo. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ikisaidiwa

kwa karibu zaidi na Halmashauri ambazo zinaonekana zipo mbele katika kukusanya mapato tu lakini si katika juhudi za kulinda na kuhifadhi mazingira.

5. Ukosefu wa Nyumba ya Makaazi kwa Mhe Makamo wa Kwanza wa Rais huko Pemba.
6. Tatizo la usafiri kwa Makamo wa Kwanza wa Rais.
7. Tatizo la Unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI:**

1. Ni busara kwa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Pemba ikaongezwa ili kuiwezesha Ofisi hiyo kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

2. Kutokana na umuhimu wa utekelezaji wa kazi katika Ofisi hii, likiwemo suala la ufuatiliaji wa uharibifu wa mazingira, Serikali inahitajika kuchukua jitihada za makusudi kwa kuipatia Idara ya Mazingira Pemba usafiri wa kutosha na wa uhakika. Vyenginevyo uhaba wa usafiri na mafuta unapelekea ongezeko la uharibifu wa mazingira pamoja na kuongezeka umaskini katika jamii.

3. Marekebisho ya Sheria ya Mazingira, ambayo kwa muda mrefu iliahidiwa kuwa itawasilishwa Barazani, inahitajika kuwasilishwa Barazani katika mwaka huu 2014 ili kuiwezesha Idara ya Mazingira kufanya shughuli zake lakini vile vile kukusanya kodi iliyokosekana.

4. Serikali ni vyema ikaongeza fungu kwenye bajeti ya Idara ya watu wenye ulemavu kwa mwaka ujao 2014/15 ili kuweza kuwanunulia vifaa vya kusomea hasa watoto wenye ulemavu wa uoni pamoja na usikivu, ikiwemo *computer,* madaftari na mashine za lugha ya alama n.k.

5. Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma itekeleze ahadi aliyoitoa Waziri hapa Barazani kwa kuwatengea nafasi maalum za ajira watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kujitegemea.

6. Kamati inaona kuna haja ya kuangaliwa sheria zote ikiwemo ya ardhi, mazingira na nyenginezo katika suala zima la utekelezaji wa miradi kwa lengo la kuzuia athari zinazojitokeza hivi sasa katika miradi ikiwemo uharibifu wa mazingira.

7. Kamati imeshauri kuwepo na sheria kwa makampuni ya uchimbaji wa vifusi ili kuweza kudhibiti hali hatarishi iliyopo hivi sasa pamoja na kuwekwa kiwango maalum cha uchimbaji huo.

**MAAGIZO YA KAMATI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS/ SERIKALI**

1. Kamati inamtaka Waziri anayeshughulikia masuala ya Ardhi kutoa maelezo ya kina na ufafanuzi ndani ya Baraza hili juu ya mmiliki halali wa eneo linalotarajiwa kujengwa kituo cha kubadilishia tabia (*Rehabilitation Centre*) huko Tunguu.

2. Serikali kupitia Idara ya Mazingir kuhakikisha miradi yote ya Serikali na ya watu binafsi inafanyiwa tathmini ya kimazingira kabla ya kuanza kwake, ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, hoteli na miradi mingine mikubwa ya ujenzi.

3. Kamati inaitaka Idara ya mazingira ishirikiane na Bodi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ili bidhaa zinazoingizwa ziwe kwenye viwango vizuri kimatumizi na kiafya kwa wananchi.

4. Sheria ya mazingira iharakishwe kuletwa Barazani ili mianya yote ya uharibifu wa mazingira iweze kuzibwa.

5. Suala la usafiri kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, Kamati inatoa agizo la kutatuliwa tatizo hilo haraka iwezekanavyo.

6. Kamati inaagiza kuwepo utaratibu maalum wa kushughulikia bidhaa chakavu zinazoingizwa nchini ikiwa ni pamoja na kuzingatia ubora wake na inapotokea kuviangamiza basi wataalamu husika washirikishwe ipasavyo.

7. Kamati inatoa agizo kwa ZIPA kuacha tabia ya kuweka mbele maslahi yao binafsi balii waweke maslahi ya nchi kwanza na kuwajibika katika kutekeleza na kusimamia sheria ipasavyo, Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hupewa vibali hata kabla ya kufanyiwa tathmini ya kimazingira jambo ambalo ni kinyume na sheria.

8. Kamati inaagiza kufanywa kwa utafiti utakaowajumuisha wataalamu wa serikali kukaa na kuangalia kitaalamu zaidi juu ya matumizi sahihi ya eneo la Kisauni ambalo lilikuwa likichimbwa Kifusi kwa faida ya nchi na watu wake.

9. Aidha Kamati inaiagiza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kushirikiana kikamilifu na Idara ya Mazingira katika shughuli zao kwa maslahi ya Umma.

## SEHEMU YA TATU

### HITIMISHO

Kwa ujumla Kamati imeweza kufanikisha majukumu yake kwa kufatilia utekelezaji wa kazi katika Taasisi zilizoainishwa katika ripoti hii kwa ufanisi mkubwa. Kamati pia inashukuru jitihada zinazochukuliwa na Taasisi hizo katika utekelezaji wa kazi zao ambapo Kamati imeweza kutoa maelekezo, ushauri na maagizo ambayo inaamini yataweza kusaidia kutekeleza majukumu ya Serikali kwa ufanisi kupitia Ofisi ya Rais,Ikulu na Utawala Bora, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Pia kamati inatoa shukrani kwa wale wote waliofanikisha kazi za kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na pia kuwezesha taarifa ya kamati kutaarishwa na kuwasilishwa kunakohusika. Kamati inamshukuru kwa dhati Mhe Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, watendaji wote wa Serikali, Watendaji wa Baraza la Wawakilishi na wote waliofanikisha kazi za Kamati.